



# Haki za Binadamu katika British Columbia: Nini unahitaji kujua



Karatasi hii ya ukweli imetengenezwa ili kukusaidia kuelewa haki za binadamu katika BC. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu hali yako, tafadhali wasiliana na **BC Human Right Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu)**. Maelezo zaidi kuhusu mawasiliano yanapatikana mwishoni mwa karatasi hii ya wa ukweli.

British Columbia ina sheria ya kulinda na kukuza haki za binadamu. Hii inaitwa *BC Human Rights Code au Code (kanuni)*. Hapa BC, *Code (kanuni)* husaidia kukulinda dhidi ya ubaguzi na unyanyasaji. Inakuruhusu kuripoti lalamiko kwenye **BC Human Rights Tribunal (mahakama ya Haki za Binadamu ya BC)** ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa.

*Code (kanuni)* hii pia inakulinda dhidi ya **kulipizwa kisasi** ikiwa umeripoti, au unafikiria kuripoti, lalamiko au umehusika kwa njia yoyote ile. **Kulipiza kisasi** ni kama kuna mtu anajaribu kukudhuru au kujaribu kukufuatilia kwa nia ya kukudhuru au kukulipiza.

## \* Namna gani ninalindwa?

Hapa BC, wewe unalindwa kwa sheria ya *Human Rights Code* iwapo inatokana kwa sababu ya sifa binafsi ambazo zimetajwa katika *Code (kanuni)*. Sifa zinazo lindwa ni hizi hapa chini.

Hapa BC ni kinyume cha sheria kubagua au kunyanyasa mtu kwa sababu ya:

- umbari, rangi, ukoo, sehemu ulipotokea
- Dini
- Hali ya ndoa
- Hali ya familia (haihusikani na kununua mali)
- Ulemavu wa kimwili au kiakili
- Jinsia (pamoja na kuwa mwanaume, mwanamke, baina ya jinsia zote mbili au aliebadili jinsia. Pia inajumuisha ujauzito, kunyonyesha, na unyanyasaji wa kingono)
- Maelekeo ya kingono ( inajumuisha kuwa na wapenzi wa jinsia tofauti, mashoga, wasagaji au wanaovutiwa na jinsia zote mbili)
- Umri ( 19 na kuendelea, haihusikani na kununua mali)
- kutiwa hatiani ya jinai (inatumika tu kwenye kuajiriwa)
- Maelekeo ya kisiasa ( inatumika tu kwenye kuajiriwa)
- chanzo halali cha mapato (inatumika tu kwenye upangaji)

## \* Code(kanuni) inatumika wapi?

*Code (Kanuni)* inatumika katika aina zote za biashara, mashirika, na aina za huduma katika BC, isipokuwa zile zinazo simamiwa na serikali ya shirikisho. Ambao inalinda watu kutokana na ubaguzi katika mazingira yao kama vile kazini, dukani au mgahawani, au kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

Ina linda watu dhidi ya ubaguzi katika machapisho. Na pia hulinda watu katika maeneo ya kazini, kukodisha, na katika ununuzi wa mali.

## \* Ubaguzi ni nini?

Katika British Columbia, ubaguzi ni kutendewa vibaya au kukataliwa mafao kwa sababu ya sifa binafsi.

### Mifano ya ubaguzi

- Mwanamke kufukuzwa kazi kwa sababu ujauzito
- Kukataa kukodisha nyumba kwa watu wawili kwa sababu wao ni mashoga.
- Kukataa kuajiri mtu kwa sababu ana ulemavu wa kimwili au kiakili
- Mwanamke kulipwa kidogo kuliko mwanaume hali ya kwamba wanafanya kazi hiyo hiyo
- Kulazimisha mfanyakazi kustaafu kwa sababu ya umri wake.

## \* Unyanyasaji ni nini?

Unyanyasaji ni aina ya ubaguzi. Inaweza kuwa maneno au vitendo vya kushambulia au kudhalilisha. Ni unyanyasaji ikiwa kuna mtu anarudia mara kwa mara anakusema au anakufanyia mambo ya kutukana na ya mashambulizi. *Code (Kanuni)* inakulinda pale ambapo unyanyasaji unapodhihirishwa kulingana na sifa zinazolindwa, ambazo zimetajwa chini ya kifungu "Namna gani ninalindwa". Kuna aina nyingi za unyanyasaji.

### Mifano ya unyanyasaji

- Mapendekezo au maombi ya kingono yasiyo kubalika
- Kuguswa au kushikwa mwili pasipo kubalika
- kukodoa macho au kutoa maoni yasio kubalika kuhusu mwili wa mtu mwingine.
- Kufanya mzaha kuhusu jinsia, mwelekeo wa kingono au ubaguzi wa kimbari au rangi.
- Kutoa maoni au kufanya utani au kutukana watu kwa sababu ya jinsia yao, ujauzito, umbari au ulemavu wa kimwili au kiakili.

## \* Nini wajibu wa kujumuisha watu wengine?

Waajiri, wenye nyumba, na watu ambao wanatoa huduma za raia lazima wafanye bidii ya kujumuisha watu wenye sifa tofauti za kibinafsi zinazo lindwa na *Code (Kanuni)*. Hii inaitwa **wajibu wa kujumuisha**. Kujumuisha kwa kutegemea na hali maalum.

Kwa mfano, mwajiri anaweza kuhitajika:

- kumpa mtu mafunzo zaidi
- kurekebisha ratiba ya kazi
- kurekebisha au kununua vifaa
- kubadilisha majukumu ya mfanyakazi

**Wajibu wa kujumuisha** pia ina maana ya kuwa kuna wajibu wa kisheria wa kurekebisha sera, utendaji au huduma. Kwa mfano, mahitaji ya mtu mzee yanayotakiwa ni kufanya mabadiliko na kurekebisha njia

za kawaida za utendaji kwa sababu ya umri wa mtu huyo. Kukataa kuchukua hatua za kutosha inaweza kuwa ubaguzi, bila kufanya marekebishi ya mahitaji hayo itasababisha **ugumu usio kuwa na maana**.

**Wajibu wa kujumuisha** ni jukumu la kila mwajiri, mwenye nyumba, au kwa yeyote mwenye kutoa huduma kwa raia.

### \* Je, kuwa na makusudi inajalisha nini?

Ubaguzi sio lazima uwe wa **maksudi** ili iwe kinyume cha sheria. Kwa maana kwamba ikiwa mtu alitenda au alitoa maneno bila ya kuwa na nia mbaya ya kufanya hivyo, ni ubaguzi kwa mujibu wa sheria.

### \* Nitajuaje kama nina malalamiko ya Haki za Binadamu?

Kuripoti malalamiko kwenye *BC Human Rights Code (Kanuni ya haki za binadamu BC)*, **yote yafuatayo** lazima yawe ya kweli:

- ✓ umetendewa ubaya au umenyimwa mafao.
- ✓ kuna uhusiano baina ya namna ulivyotendewa (vibaya au kunyimwa mafao) na sifa zako za binafsi zinazolindwa katika *Code (kanuni)* - kama umbari, rangi, imani za dini, jinsia, ulemavu wa akili au mwili, au mwelekeo wa kingono.
- ✓ Vitendo hivyo viwe vimetokea katika sehemu kama vile kazini, dukani au mgahawani, au baina ya mwenye nyumba na mpangaji.

Lazima uripoti malalamiko yako katika muda wa miezi sita ya tukio kutoka. (Kumbuka: kuna baadhi ya kesi za kipekee zisizo fuata muda huo uliyowekwa.) Kuripoti malalamiko kuanzisha mchakato wa kisheria sawa na hatua za hakama. Mtu mwenye kuripoti malalamiko anaitwa **malalamikaji**.

### \* Kukabiliana na ubaguzi na unyanyasaji

Kuna baadhi ya hatua unayoweza kuchukua ikiwa umebaguliwa au unenyanyaswa.

- Ikiwa kuna usalama kuchukua hatua hizo, mwambie huyo mtu kwamba vitendo hivyo na maneno hayo siyo mazuri na pia mwambie asiendeleeze.
- Hifadhi kumbukumbu ya yaliyotokea, yaliyosemwa na wakati gani kwa maandishi.
- Ikiwa ubaguzi au unyanyasaji umetokea kazini, kwenye nyumba unayokodisha, au kwenye duka au mgahawa, muombe muajiri wako au mwenye nyumba au meneja achukue hatua.
- Tumia mchakato wa sehemu hiyo uripoti malalamiko yako kazini au shuleni. Kwa mfano, ikiwa ubaguzi au unyanyasaji umetokea kazini na wewe ni mwanachama wa muungano, omba msaada kwa mwakilishi wa muungano huo.

### \* Wapi naweza kupata usaidizi?

**Walalamikaji** popote katika jimbo wanaweza kupata maelezo kupitia **BC Human Rights Clinic (Kilinki ya BC ya Haki za Binadamu)**. Watu wa kliniki wanaweza kukusaidia kuelewa *Human Rights Code (Kanuni za Haki za Binadamu)* au kushughulikia malalamiko ya haki za binadamu ya jimbo. Unaweza pia ukafuzu kupata aina tafauti za huduma. Zungumza na mtu yoyote katika kliniki ili uone ikiwa utakubaliwa.

### Kilinki ya BC ya Haki za Binadamu

300-1140 West Pender Street, Vancouver, B.C. V6E 4G1  
Phone: 604 622-1100 Toll Free: 1 855 685-6222  
Fax: 604 685-7611  
Online: [www.BCHRC.net](http://www.BCHRC.net)

Ikiwa kuna mtu amefanya malalamiko juu yako, basi wewe ni **mhojiwa**. **Wahojiwa** wote kwenye jimbo na eneo la Victoria wanaweza kupata maelezo zaidi kwa kuwasiliana na:

### University of Victoria

Law Centre Clinical Law Program  
Suite 225 – 850 Burdett Avenue, Victoria, B.C. V8W 1B4  
Phone: 250 385-1221 Toll Free: 1 866 385-1221  
E-mail: [reception@thelawcentre.ca](mailto:reception@thelawcentre.ca)

Unaweza kuelekezwa kwa **BC Human Rights Tribunal (Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu)** kuwasilisha malalamiko yako.

### Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu

Suite 1170 – 605 Robson Street, Vancouver, B.C. V6B 5J3  
Phone: 604 775-2000 Toll Free: 1 888 440-8844  
TTY (walio kuwa na matatizo ya kusikia): 604 775-2021  
Online: [www.bchrt.gov.bc.ca](http://www.bchrt.gov.bc.ca)

*karatasi hii ya maelezo imekusudiwa kwa madhumuni ya kutoa maelezo kwa ujumla tu. Sio kwa nia ya kuchukua nafasi ya ushauri wa kisheria.*